**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI NASULI**

# FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)

**Namba za Simu**
**Mkuu wa Shule 0653136005/0783077050**
**Makamu Mkuu wa Shule 075233170**
**Mtaaluma 0717709592**

**Shule ya Sekondari NASULI**
**S.L.P 21**
**NAMTUMBO-RUVUMA**
**Tarehe 01/06/2026**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

YAH**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NASULI ILIYOPO KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA NAMTUMBO MKOA RUVUMA**

**1.0** Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha Tano katika shule hii kwa mwaka 2026/2027. Shule hii ipo kilometa 68 mashariki mwa mji mkuu wa mkoa wa Ruvuma (Songea) na Kilometa 185 magharibi mwa wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma. Usafiri wa Basi toka Songea mjini unapatikana kituo cha Mabasi Songea, nauli ni Tshs 5.000/=. Ukifika Namtumbo teremka katika kituo kikuu cha mabasi cha Namtumbo na shule yetu ipo upande wa pili wa barabara. **UNATAKIWA KURIPOTI SHULENI KUANZIA TAREHE ……....... HADI TAREHE…......** Mwanafunzi atakae chelewa kuripoti kwa tarehe hiyo, nafasi yake atapewa mwanafunzi mwengine.

**2.0 Mwanafunzi aje na vitu vifuatavyo:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Aje na shati nyeupe mbili mikono mifupi (Mashati mawili au zaidi)
ii. Aje na sketi ya rangi ya Kijani iliyoiva (dark green) yenye rinda box mbele na nyuma yenye urefu hadi kwenye kifundo cha mguu (ankle) (Sketifupi HAZIKUBALIKI). Kwa atakayependa zinapatikana karibu na shule kwa gharama ya Tsh.30, 000/= kwa sketi moja.
iii. Aje na viatu vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
iv. Aje na soksi nyeupe (jozi mbili).
v. Aje na sweta la shule rangi ya kijani iliyoiva (dark green). Kwa atakayependa inapatikana karibu na shule kwa Tsh.15,000/=
vi. Aje na nguo za kushindia, (Shamba dress) ni Gauni rangi ya damu ya mzee, mshono ni solo ndefu lifike kwenye vifundo vya miguu. Kwa atakayependa zinapatikana karibu na shule kwa Tsh.35,000/= kwa gauni moja.
vii. Aje na Hijabu ifanane na sare za shule (Nyeupe na Damu ya mzee sio mtandio isiwe na urembo wala lessi).

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASULI
NAMTUMBO

viii. Kwa waislamu, aje na nguo ya Kusalia -suruali dark blue ya heshima na isibane -nusu kanzu ndefu ipite magoti na yenye mikono mirefu.
ix. Aje na sare ya michezo, traksuit nyeusi zenye michirizi nyeupe pembeni na raba nyeupe. Kwa atakayependa,Track suit zinapatikana karibu na shuleni kwa Tsh.25,000/= .
x. Aje na Tshirt sare ya shule yenye kola rangi ya damu ya mzee. Kwa atakayependa zinapatikana karibu na shule kwa Tshs 15,000/=

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari yasiyopungua 10 quire three kwaajili ya kutunzia notes na daftari aina yoyote kwaajili ya mazoezi kwa kilasomo.
ii. Mkebe wenye vifaa vya mahesabu.
iii. Rimu 2
iv. Kalamu za wino bluu/nyeusi, yaani 01 kila mhula, faili 01 kwa ajili ya kutunzia nyaraka zake, scientific calculator kwa wanaosoma masomo ya sayansi, dissecting kit (kwa wanaosoma Biology) na koti la maabara jeupe (kwa wanaosoma CBG na PCB), na Advanced English Dictionary kwa wanafunzi. Kwa atakayependa Calculator inapatikana karibu na shule kwa Tsh.30,000/=. Pia mwanafunzi afike na Vitabu vinavyoendana na masomo yake kwa ajili ya kujisomea.
v. Aje na sanduku (sanduku la bati ) linalofunga vizuri kwaajili ya kuhifadhia nguo zake na vitu vyake.
vi. Aje na godoro la futi 21 / 2 kwa futi 6 pamoja na mto na foronya yake
vii. Aje na blanketi 01, shuka rangi ya bluu bahari 02, pinki 01, chandarua rangi nyeupe/bluu 01 na taulo 01.
viii. Aje na vifaa vifuatavyo:
- Jembe jipya lenye mpini 01
- Kwanja 01
- Panga 01

Fagio (chelewa) 02 na soft bloom 01, hard bloom 01na brashi ngumu 01yenye mpini mfupi kwaajili ya kusafishia sinki la choo

ix. Aje na Ndoo ya lita kumi mbili (02) na Squeezer 01 kwaajili ya kukaushia maji sakafuni
x. Aje na Dumu la lita tano (05) ya sabuni ya maji kwaajili ya usafi.
xi. Aje na nakala ya leaving certificate, matokeo ya kidato cha nne (result slip) na cheti cha kuzaliwa.

**2.3 Michango mbalimbali Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Fedha za michango zilipwe kwenye akaunti ya shule namba **0152366830400** Jina la akaunti (SHULE YA SEKONDARI NASULI) benki ya CRDB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya kuwekea hela (paying slip) na iletwe shuleni siku atakayoripoti mwanafunzi.

Aje na Tsh **50,400**/= kwa ajili ya bima ya afya kwa mwaka mzima (kwa wale ambao hawana bima ya afya). Ni muhimu sana kwani itamsaidia kutibiwa kwa mwaka mzima sehemu yoyote

nchini.(fedha hizo siyo sehemu ya michango ya shule, hivyo alete fedha taslimu. Asiingize kwenye akaunti ya shule)

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASULI
NAMTUMBO

**3.0 Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamo jana;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shule ni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtu mishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.**
- **Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupiga na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababishamimba;
xiii. Kushiriki matendo yauhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera yaTaifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4.0 Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine ya na yotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.0** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule**

**Jina la Mkuu wa Shule ANNA VINCENT MBAWALA**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SECONDARI NASUI
NAMTUMBO

**Mhuri wa Mkuu wa Shule ………………………………..**

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

- **Mkuu wa shule 0783077050**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0752331702**
- **Mwandamizi Taaluma 0717709592**
- **Mwandamizi Malezi 0713452298**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SECONDARI NASULI
NAMTUMBO

**Kiambata ''A''**

## FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NASULI

**A. Sehemu ya mwanafunzi**

Mimi……………………………………………………………………………… Ninakubali nafasi niliyopewa kuingia kidato cha tano kwa mwaka………………katika shule ya sekondari Nasuli na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na Nchi.Ninaahidi kutoshiriki katika mgomo,fujo na makosa ya jinai.Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za Elimu ya kujitegemea.

Anuani yangu ya kudumu ni…………………………………………………………

……………………………………………….

………………………………………………

………………………………………………

Sahihi………………………………………. Tarehe……………………………………

**B. Sehemu ya Mzazi/Mlezi**

Mimi………………………………………………………………….ninakubali

Mtoto wangu…………………………………………………. Kuchukua nafasi ya kuingia Nasuli sekondari kidato cha tano mwaka……………………………Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule.Pia nakiri kukubaliana na sheria,kanuni za shule pamoja na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa.

Anuani yangu ya kudumu ni

………………………………………………………….

…………………………………………………………..

…………………………………………………………

Iwapo nitapata uhamisho au kubadili makazi,ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi
Sahihi…………………………………………………………………
Tarehe…………………………………………….

MKUU WA SHULE
SHULE YA SECONDARI NASULI
NAMTUMBO

**Kiambata ``B''**

**TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI**

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika Kidato cha Nne ……………………………………
2. Shule ya Sekondari uliyo soma…......................................……………………………..
3. Dini yako /dhehebu…………………………………………………………..…………….
4. Jina kamili la baba mzazi/ mlezi……………………………………………………….

   Kazi yake………………………………………………………………………………

   Anuani kamili ya baba mzazi/mlezi………………..…………………………………….

   Na.yake ya simu ya mkononi…………………….………………………………………

   Na. yake ya simu ya mezani………………………………………………………...

   Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi: Mkoa…………….… Wilaya……………………

   Tarafa……………………………………Kata……………………………………….

   Kijiji/ Mtaa………………………….

5. Jina kamili la mama mzazi /mlezi……………………………………………………

   Kazi yake………………..……………………………………………………………..

   Anuani kamili ya mama mzazi / mlezi…………………………….……………………

   Na. yake ya simu ya mkononi…………………………………………………………..

   Na. yake ya simu ya mezani…………………………………………………………….

   Mahali anakoishi mama mzazi /mlezi……………………………………………………

   Mkoa……………………………Wilaya………………………………………………

   Tarafa…………………………………kata…………………………………………

   Kijiji / Mtaa……………………………………..

MKUU WA SHULE
SHULE YA SECONDARI NASUI
NAMTUMBO

**Kiambata “C”** **THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRIME MINISTER `S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENTS**

NASULI SECONDARY SCHOOL,
P.O. BOX 21,
**NAMTUMBO,**
01/06/2026

DISTRICT MEDICAL OFFICER,
POBOX………………………,
Dear Sir / Madam.

**Re: A REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.**

Please examine Mr. /Miss ………………………………………………..as to his /her physical and mental fitness for admission as a Form one student at Nasuli secondary school in the year 2021.

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI NASULI
NAMTUMBO

Yours sincerely,

…………………………..

**ANNA VINCENT MBAWALA**
**HEADMISTRESS**

---

The Headmistress,

I have examined Mr/ Miss…………………………………………as shown below and consider that he/she is physically and mentally fit/unfit for admission to pursue a full time secondary education.

1. Vision with /without glasses. Right………………………. Left………………
2. Blood pressure……………………… Haemoglobin……………………………
3. Hearing………………………………………………………..
4. Urine (a) ……………………………………………………….

5(a) Venareal diseases ………………………………(b) Bilharzia……………………

6. Pregnancy………………………………………………………..
7. Neurosis………………………………………………………
8. Is there any abnormality of?

(a) The heart………… (b) Lungs………(c) The spleen…………………………

9. Are there any serious diseases e.g. Leprosy, epilepsy, asthma, diabetes etc.
…………………………………………………………………………………………

Any comments……………………………………………………………………………

Date............................................. Signature of Medical officer ………………………..

Station……………………………… Designation…………………………………………

**Kiambata “D”**

Rangi za uniform, Sketi, Shamba dress na Sweta

Sketi ya Shule



Track suit Nyeusi



Shamba Dress



Jezi ya Michezo/kushindia




Sweta



MKUU WA SHULE
SHULE YA SECONDARI NASUI
NAMTUMBO